

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MADINI**

TUME YA MADINI

Telegram "MADINI"

Simu: +255 26 2320051

Nukshi: +255 26 2322282

Baruapepe: ceo@tumemadini.go.tz



S.L.P. 2292,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Tume ya Madini kwa Mujibu wa Kanuni Namba 6(2)(b) ya *The Mining (Local Content) Regulations, 2018* inawataka waombaji na wamiliki wote wa leseni za utafutaji, uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini kuwasilisha Mpango wa Ushirikishwaji wa Utoaji Huduma na Bidhaa kwa wazawa katika Miradi ya Madini.

Kutokana na Kifungu cha 106(3) cha Sheria ya Madini, Tume pia inawataka waombaji na wamiliki wa leseni hizo kuwasilisha tamko la Kiapo cha Uadilifu (*Integrity Pledge*). Miongozo ya nyaraka hizo inapatikana katika tovuti ifuatayo:- www.tumemadini.go.tz na www.madini.go.tz.

Kwa vile uchambuzi wa maombi umeshafanyika, hivyo utoaji wa leseni hizo utafanyika pindi tu waombaji watakapowasilisha nyaraka tajwa.

Imetolewa na:

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Prof. Idris Kikula'.

Prof. Idris Kikula

MWENYEKITI

Julai 17, 2018